TAREKHE YA SHARIF SAID AL-BEIDH

1 SHAABAN 1330h – 28 MUHARRAM 1383h.

RADHI YA ALLAHU IWE NAE, AAMIN.

Kwa munasaba wa ukumbusho wa Kiongozi wetu Mwanachuoni Al-habib Assayyid Asharif Said bin Abdallah bin Said Al-beidh unaosimamishwa killa mwaka ikiwa mwaka huu (1423h – 2002) ni wa arubaini, tumependa kuieleza tarekhe yake kwa ufupi sana ili ajulikane yeye ni nani katika uislamu.

Sharif Said ni miongoni mwa silsila ya kizazi cha Bwana Mtumi Muhammad (S.A.W.) wanaojulikana kwa Masharifu, Babake ni katika kabila la Al-beidh na Mamake ni Jamalullayli alizawa katika mji wa Malindi Kenya, mwando wa Shaaban mwaka 1330h, alipata malezi ya kwanza mema kutoka kwa wazazi wake wawili

(babake na mamake) na akainukia kwa kupenda Dini na ilimu na watu wema na alikua na malezi mazuri na twabia njema.

Na katika mwaka 1344h aligura kutoka Malindi kwenda Lamu kwa maombi ya Babu yake Al-habib Swaleh na Lamu alilelewa na Mjombake Al-habib Ahmad Badawiy (Mwenye Badawi) chini ya uongozi wa Babu yake Al-habib Swaleh na pia alisoma kwa Mashekhe na Wanazuoni mbalimbali wa Lamu na miji mingine khaswa khaswa Wajomba zake na pia alijifundisha ilimu ya utwabibu hata akawa ni mtegemewa mkubwa na hodari asiekurubiwa na yeye ndie wa kwanza alieweka mpango wa kimadrasa unaoendelea huku kwetu hadi sasa na ilikuwa kabla ya kufunguliwa Madrasatu Nnajahi Lamu mwaka 1357h.

Na alipofika miaka 26 (1356h) alisafiri pamoja na Mjombake Mwenye Badawi kwenda Hadhramout na huko alipata dua na ijaza nyingi kutoka kwa Masharifu na Mashekhe mbali mbali, na

mwaka (1357h) ndio ilikua safari yake ya kwanza kwenda Hijjah pamoja na Mjombake na pia akakutana na Wanazuoni tofauti tofauti na akatunukiwa dua na ijaza.

Baadae Sharif Said alifanya biashara aina mbali mbali alifungua duka kubwa (whole sale) Lamu hata akahisabiwa ni mfanya biashara mashuhuri, pia alilima mashamba sehemu tofauti tofauti Lamu, Witu na Mambrui, na yote hayo alifanya kwa ajili ya kuweza kujitegemea mwenyewe bila ya kumuhitajia mtu yoyote na ilikuwa hakuna jambo analolitukia zaidi kuliko kuomba au kuombewa.

Baadae alianza kazi ya jihadi na daawa kama ada ya mababu zake wema waliotangulia, akajitolea muhanga kuingia kwenye majabali, mapango, na sehemu zisizofikiwa na watu wingi kwa ajili ya daawa tu bila ya kujali lolote.

Safari yake ya kwanza ya mbali ilikuwa ni kwenda magharibi mwa mtu nile (Uganda) kwa kupitia Tanganyika (Tanzania Bara) mwaka wa 1363h, na

alikuwa akipendekeza sana kila pahali ashukiapo kwa ukweli wake na twabia yake njema na juhudi zake za kushukuriwa, alikuwa ni mwenye hikma kubwa katika daawa yake, akipenda watu wote na akiwaweka sawa sawa bila ya ubaguzi wowote, kisha alifungua duka katika mji wa Warr (Wadi Rridha) kwa ndia ya daawa ikawa killa mwenye kununua sukari mathalan humpa mayani bure na mwenye kununua chochote humpa kingine bure, mpaka akaulizwa "je waridhia khasara katika biashara yako?" akajibu " mimi sifanyi biashara wala sina haja nayo lakini ni daawa kwa mavazi ya biashara".

Baada ya kujitolea kwa jihad na daawa na kukumbana na taabu na shida na mashaka na kusubiri balaa na udhia alisilimisha maelfu ya watu bali alisilimisha baadhi ya makabila ambayo yalikuwa hayana muislamu hata mmoya kama kabila la Alur mwaka wa 1372h na waislamu wingi wa magharibi wa mto nile walisilimishwa na yeye, mpaka sasa pamoja

na kutangamanisha na zizazi zao na kukunduka kwa daawa yake ni zaidi ya watu laki tatu waloingia kwenye uislamu kwa ajili yake, Mola amjazi kheri.

Aliasisi Miskiti na Madrasa nyingi sehemu mbali mbali na baadhi ya Miskiti alijenga yeye mwenyewe kwa mkono wake kama Msikiti wa Warr na Miskiti miwili Aringa, ama Miskiti na Madrasa alizozisimamia hazina hisabu nchini Uganda na Kenya, khaswa khaswa Masjidi Riyadh Mambrui Ambao aliukundua na akaurakibisha, na kadhalika Madrasatu Nnuri (Mambrui) alikuwa ni msimamizi mtegemewa na mshauriwa asiepingwa.

Alikuwa Sharif Said ni mtumishi wa kujitolea kwa kuwasaidia umma kwa hali na mali khaswa khaswa kwa umahiri (uhodari) aliokuwa nao wa kiutwabibu na kwa dawa za kiajabu alizokuwa akiwafanyia wagonjwa, mpaka alidhihirisha uhodari wa kumtibu mgonjwa kwa kutumia sumu na akapoa, na hili ni katika karam zake, na utwabibu wake ni wa hali ya juu

sana mpaka sirikali ya Uengereza ikampa shahada ya kumkubali kwa uhodari wake, na dawa zake sana alikuwa akizitowa bure kwa kusaidia umma na ni nadira kutofaulu utwabibu wake.

Na ilikuwa kuwasaidia watu ndio umbile lake na dasturi yake kwa ndia tofauti tofauti hakiweki kinachozidi na hamrudishi mwenye kuhitaji hata alisema katika maneno yake " safari yangu kutoka Arua mpaka Lamu ni yenye gharama nyingi zaidi kuliko safari yangu ya kwenda hijja " akaulizwa " kwa nini?" akasema " safari yangu ya hijja yanilazimu nauli na haja za nafsi yangu tu, ama safari yangu ya kutoka Arua kwenda Lamu sipiti kwenye mji wowote ila huwasaidia wenye kuhitajia kwangu usaidiza nao ni wingi".

Na alikuwa kawaida yake ni kulisha chakula cha usiku idadi ya watu 30 hadi 100 popote anapokuwepo kwake, na lipokufa alikuwa hana cha kurithiwa ila ni kipande cha ardhi kinachofika ekari mbili

na akawata jumla ya 1750/= hizi tu ndizo zilikuwa wirathi wake.

Alikuwa Sharif Said ni hodari sana kwa kupika, alikitengeza biskoti, na chakleti, na akitengeza zakula 12 mbali mbali kutokana na muhogo, na alini mjengaji bora, na mekanikani hodari na mpekaji gari na mtengezaji saa na muindaji mzuri sana mwenye shabaha, alikilenga ndege wawili kwenye anga kwa risasi moja, na alikuwa akitembea mwendo mrefu zaidi, aliwahi kutoka Malindi hadi Lamu (220 km.) kwa baskili mara saba na huku amepakia mtu mmoja au wawili, ama kwa miguu ni bila idadi.

Na alikuwa Sharifu pamoja na hayo yote ni mcha Mungu, mpanyongo dunia, mkeshaji kwa ibada, mkarimu, mwenye haiba ya imani na nuru ya ucha Mngu, mwenye karama za wazi wazi zilizoshudiwa na watu wingi (hata mazishi yake yalikuwa ni ya kikarama), hana haja ya cheo au jaha ya duni.

Aliwahi kuhiji hijja tisa na akafa wakati yuwarudi kutoka kwenye hijja yake ya mwisho kabla ya kufika nyumbani kwake kwa sababu ya kupinduka kwa gari walilokisafiria pahali panapojulikana kibao cha Takaungu siku ya juma nne tarekhe 25 akapandishwa hospitalini na akaugua siku tatu tangu apenduke na alikuwa akiusia na akiaga watu, na akafa usiku wa ijumaa tarekhe 28/Muharram/1383h na akazikwa Mambrui kama alivyousia na lipata mazishi ya kiajabu na watu wengi mno.



KUBBA LA SHARIFF SAID

KUONYESHA UTUKUFU WAKE NA KUTHIBITISHA KWAMBA NI MTU MWEMA NI KUWA KATIKA UHAI WAKE NA MPAKA SASA HAKUNA ALOMTIA DOA LA AINA YOYOTE ILA WASOTHAMINIWA